# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

## MKUTANO MKUU WA 40 WA MWAKA WA JUMUIYA YA WAHITIMU

## KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA 40 WA MWAKA WA JUMUIYA YA WAHITIMU ULIOFANYIKA TAREHE 16 NOVEMBA, 2018 KATIKA CHUMBA NA. B106 KATIKA SHULE KUU YA BIASHARA KUANZIA SAA 3.00 ASUBUHI

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**
Orodha imeambatanishwa

**KUFUNGUA MKUTANO**

Mwenyekiti alifungua mkutano saa 3:36 asubuhi baada ya kuthibitisha akidi.

**KUIKUBALI AJENDA**

Ajenda ya mkutano ilikubaliwa kama ilivyowasilishwa.

**DONDOO NO. 1 KATIKA AJENDA: KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA 39 WA MWAKA WA JUMUIYA YA WAHITIMU ULIOFANYIKA TAREHE 27 NOVEMBA, 2009 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA BARAZA LA CHUO KUANZIA SAA 3.00 ASUBUHI**

**KUMB NA. 317**

317.1 Kumbukumbu za mkutano wa 39 wa mwaka wa Jumuiya ya Wahitimu **ZILITHIBITISHWA.**

**DONDOO NO. 2 TAARIFA YA KAZI YA OFISI YA JUMUIYA YA WAHITIMU KWA KIPINDI CHAKUANZIA NOVEMBA 2009 MPAKA NOVEMBA 2018.**

**KUMB.NA. 318**

318.1 Mkutano **ULIZINGATIA** taarifa ya kazi mbalimbali zilizofanyika na ofisi ya Jumuiya ya Wahitimu kwa kipindi cha miaka tisa (9).

318.1.1 Mkutano **ULIPONGEZA** kazi nzuri zinazofanywa na ofisi ya Jumuiya ya Wahitimu lakini pia kwa Uongozi wa Chuo kwa kuendelea kusaidia kwa kila hali maendeleo ya ofisi hii.

**DONDOO NA. 3 KATIKA AJENDA: RIPOTI YA FEDHA**

**KUMB. NA. 319**

319.1 Mkutano **ULIZINGATIA** taarifa ya ukaguzi wa fedha ya kuanzia 1 Julai 2009 mpaka tarehe 30 Juni 2019.

319.1.1 Mkutano **ULIPONGEZA** maandalizi mazuri ya taarifa hiyo kulinganisha na miaka iliyopita.

**DONDOO Na. 4 KATIKA AJENDA: UCHAGUZI MKUU WA RAIS, MHAZINI NA WAJUMBE WA KAMATI TENDAJI YA JUMUIYA YA WAHITIMU**

**KUMB. NA. 320**

320.1 Mkutano **ULIPOKEA** taratibu za uchaguzi wa nafasi zote za uongozi ndani ya Jumuiya ya Wahitimu

320.2 Mkutano **ULISHIRIKI** zoezi la uchaguzi kama ifuatavyo;

320.2.1 Mkutano **ULIARIFIWA** kuwa katika nafasi ya Urais ni Mhitimu moja tu Balozi Mwanaidi Sinare Maajar aliyependekezwa na Kamati Kuu na kukubali jina lake kupigiwa kura kwenye Mkutano Mkuu wa Uchaguzi.

320.2.1.1 Mwenyekiti **ALIWAARIFU** wajumbe kuwa mjumbe aliyependekezwa alipata ajali ya kuteleza na kuvunjika mguu wa kulia hivyo aliomba udhuru.

320.2.1.2 Wajumbe wote wa Mkutano **WALIMTHIBITISHA** kwa kauli moja Balozi Mwanaidi Sinare Maajar kuwa Rais wa Jumuiya ya Wahitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka mitatu.

320.2.2 Wajumbe wanne (4) wasio watumishi wa Chuo Kikuu Dar es salaam **WALIPENDEKEZWA** kupigiwa kura na Mkutano Mkuu ili kuwapata wajumbe watatu (3) watakaoingia katika Kamati Kuu ya Jumuiya ya Wahitimu. Wajumbe waliopigiwa kura ni kama ifuatavyo;

1. Bw. Benedict Ntake - Kura 5
2. Bw. John Ulanga – Kura 34
3. Bi. Farida Hamza – Kura 41

4. Bw. John Kalage – Kura 33

320.2.2.1 Wajumbe wote wa Mkutano **WALIWATHIBITISHA** kwa kauli moja wajumbe watatu waliopata kura nyingi nao ni; Bi. Farida Hamza, Bw. John Ulanga, na Bw. John Kalage kuwa Wajumbe wa Kamati Kuu ya Jumuiya ya Wahitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

320.2.3 Wajumbe wote wa Mkutano **WALIMTHIBITISHA** kwa kauli moja Bi. Tumaini Kihunrwa kuendelea kuwa Mhazini wa Jumuiya ya Wahitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

**DONDOO. NO. 5 KATIKA AJENDA: HOTUBA YA RAIS WA JUMUIYA YA WAHITIMU ANAYEMALIZA MUDA WAKE**

**KUMB.NA. 321**

321.1 Mwenyekiti wa Mkutano **ALIWAHUTUBIA** wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Jumuiya ya Wahitimu kwa kuelezea kwa kina baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chake kama ifuatavyo;

321.1.1 Mkutano **ULIARIFIWA** kuwa juhudi kubwa ya kuanzisha Kanzi Data kwa ajili ya Wahitimu ilikuwa imefanyika na kwamba kilichobaki nikuhakikisha inatumika kikamilifu katika kuhifadhi na kuwasiliana na Wahitimu.

321.1.2 Mkutano **ULIARIFIWA** kuwa Jumuiya hii ya Wahitimu ilifanya jitihada nyingi katika kuweka wazi matatizo mbalimbali yanayokabili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama vile mabweni ya wanafunzi na nyumba za wafanyakazi.

321.1.3. Mkutano **ULIARIFIWA** juu ya malengo ya kuanzisha ujenzi wa Kituo cha Wanafunzi kuwa ni kuweza kutoa nafasi kwa wanafunzi wengi zaidi kunufaika na huduma kama za tehama na hata nafasi ya kujisomea binafsi kuliko ilivyo hivi sasa ambapo hukaa kwenye majani. Tatizo hili limekuwa likiwakumba zaidi wanafunzi ambao hawana makazi katika kampasi ya Mlimani.

321.1.3.1 Mwenyekiti **ALIPENDEKEZA** kazi zaidi ifanyike kuunganisha Wahitimu na Chuo Kikuu chao pamoja na kuwashirikisha maendeleo na matatizo mbalimbali kadri yanavyojitokeza.

**DONDOO. NO. 6 KATIKA AJENDA: MENGINEYO**

**KUMB.NA. 322**

322.1 Kwa kuwa hakukuwa na suala jingine la kujadili, Mwenyekiti alifunga mkutano saa 8.50 mchana.

Daniel Mugassa Stephen
**MWANDISHI WA KUMBUKUMBU**

Zimehakikiwa na ……………………………………………………………………
Dr. Lulu Tunu Kaaya
**MKURUGENZI WA UMATAIFISHAJI, JUMUIYA YA WAHITIMU NA UENDELEZAJI CHUO**

Zimehakikiwa pia na ……………………………………………………………
Prof. David A. Mfinanga
**NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO (UTAWALA)/KATIBU**

Zimeidhinishwa kutolewa na: ………………………………………… Tarehe: …………………………………
Balozi Mwanaidi Sinare Maajar
**RAIS WA JUMUIYA YA WAHITIMU/MWENYEKITI**

Zimethibitishwa na: ……………………………………………………… Tarehe: ……………………………………

Balozi Mwanaidi Sinare Maajar
**RAIS WA JUMUIYA YA WAHITIMU/MWENYEKITI**